

**SERA**
Serikali kutafuta suluhisho la kudumu kwa baa la njaa badala ya chakula cha msaada **UK 3**



**HAZINA**
Nafuu kwa wakazi wa Makueni baada ya bwawa la Ndukuma kukarabatiwa **UK 4**

**KILIMO**
Serikali kusambaza tani 15.8 za nafaka za pamba za BT kwa wakulima Nyanza



**UK 9**

www.mygov.go.ke

MACHI 21, 2023

TATHMINI YAKO YA WIKI

MyGov.

TOLEO No. 36/2022-2023

# KNLS kugeuza makontena kuwa maktaba kwenye maeneo bunge

Afisa Mkuu Mtendaji wa KNLS asema shirika hilo litashirikiana na shule kutambua maeneo ambayo makontena yatawekwa kukidhi mahitaji ya kusoma ya wanafunzi vijana na watu wazima katika maeneo ya mashambani

**NA MUTISO MBITHI (MYGOV)**

Shirika la Taifa la Huduma za Maktaba Kenya (KNLS) litabadilisha makontena ya chuma kuwa maktaba za muda kama hatua ya kuhudumia kaunti ndogo na maeneo bunge yasiyo na huduma za maktaba za taifa.

Afisa Mkuu Mtendaji wa KNLS Dkt Charles Nzivo alisema kwamba shirika hilo litashirikiana na shule za msingi na sekondari ili kutambua maeneo ambayo makontena yatawekwa kukidhi mahitaji ya kusoma ya wanafunzi vijana na watu wa maeneo ya mashambani kwa Wakenya na Kwa njia nafuu.

Dkt Nzivo pia aliongeza kuwa KNLS inashirikiana na Wakfu wa Nation Media Group kuwezesha ununuzi



wa makontena matupu, kutayarisha na kuyaweka maudhui ya kusoma ya humu nchini huku mmoja wa wafadhili wake wakuu wa vitabu Book Aid International ambalo limekuwa likitoa vitabu kwa shirika hilo tangu 1965, litatoa nyenzo za kimataifa za masomo kama sehemu ya ku-

ENDELEA UK 2

## Kituo cha utafiti chaunda choo cha kupiga jeki mpango wa makazi nafuu

**NA PARIN WANJIRU(PCO)**

Kituo cha Utafiti wa Ujenzi Kenya (KBRC) kwa ushirikiano na Idara ya Sanaa na Muundo ya Chuo Kikuu cha Nairobi (StAD) kimeunda kauri ya choo ya bei nafuu inayoitwa Ngisi.

Choo hiyo imeundwa kwa kutegemea udongo kutoka Mukurwe-ini, kaunti ya Nyeri na kaunti ya Makueni.

Uvumbuzi huo unanuiwa kutengeneza vifaa vya ujenzi vya choo kwa kutumia nyenzo zinazopatikana nchini ambazo zitasaidia mpango wa nyumba nafuu Kenya. KBRC, iliyo chini ya Idara ya Serikali ya Ujenzi katika Wizara ya Ardhi na Mipango ya Miji imejukumiwa kufanya utafiti na kutoa habari kuhusu jinsi nyenzo za ujenzi za bei nafuu na tekinolojia za uchumi jamii zinaweza




**Mfano wa choo aina ya Ngisi iliyotengenezwa na KBRC**

kutengenezwa Kenya.

Duru za cheo cha juu katika Idara ya Serikali zilisema jina Ngisi litatumiwa katika vifaa vingi vya ujenzi vitakavyotengenezwa baadaye.

"Ngisi ni jina ambalo limeundwa kutoka neno la Kisamburu Ngisipet kumaanisha kifaa kinachofa-

ENDELEA UK 2

**Takwimu za Wiki**

| 1,800 | 10,000 | 15B | 110m |
|---|---|---|---|
| Idadi ya watu mashuhuri ambao wataweza kukaa katika uwanja mpya wa michezo wa Embu Stadium | Wakazi wa Makueni ambao watanufaika na mpango wa kuondoa uchafu kwenye bwawa la Ndukuma | Idadi ya miche ambayo Rais William Ruto anapigania kupandwa kufikia 2023 | Kiasi cha pesa of EU ilipatia JKUAT kutekeleza mradi wa ubunifu dijitali |

## Kongamano la Kimataifa kuhusu Habari




**Katibu Mkuu wa Chama cha Kimataifa cha Tekinolojia ya Mawasiliano (ITU) Doreen Bogdan-Martin (kushoto) akiwa na Katibu wa Wizara ya Habari na Mawasiliano Prof Edward Kisiang'ani baada ya mashauriano katika mkutano wa WSIS jijini Geneva.**




# KNLS kugeuza makontena kuwa maktaba maeneo bunge

ENDELEA KUTOKA UK 1

wajibikia jamii (CSR).

Afisa Mkuu Mtendaji huyo alikuwa akizungumza katika makao makuu ya KNLS Maktaba House, Upper Hill, Nairobi, alipopokea wanachama wa Kamati ya Bunge kuhusu Utangazaji na Maktaba, waliofanya ziara ya kujifahamisha.

"Tunanuia kupanua huduma zetu za maktaba hadi kiwango cha maeneo bunge ili kuhakikisha tunainua upatikanaji wa nyenzo zetu za kusoma ambazo zinatolewa bila malipo kwa gharama ya mlipa ushuru kwa watoto wanaoenda shule na wanafunzi watu wazima,"Dkt Nzivo aliambia wabunge hao.

Waliongozwa na naibu mwenyekiti Mhandisi Kiragu Chege, mbunge wa Limuru katika Bunge la Taifa.

Hata hivyo, Dkt Nzivo alihimiza wabunge kutenga pesa kutoka Hazina ya Serikali ya Kitaifa ya Maeneo Bunge (NG-CDF) kujenga maktaba kati maeneo bunge yao kupakulia desturi ya kusoma miongoni mwa Wakenya.




Alipongeza maeneo bunge kama Eldama Ravine, Awendo, Kimilili, Kangema, Imenti Kusini na Voi kwa kufadhili kikamilifu ujenzi wa Maktaba kwa kutumia pesa kutoka NG-CDF. KNLS ni Shirika la serikali lililotwikwa jukumu la kuanzisha, kuweka vifaa kusimamia na kustawisha na maktaba katika kiwango cha eneo na kitaifa ili kupalilia desturi ya kusoma na kutoa habari za kuwezesha Wakenya. Mhandisi Kiragu alisifu uwekezaji mkubwa wa miundomsingi wa serikali kwa KNLS ambao umeiwezesha kuongeza uwezo wake wa kutoa nyenzo za kusoma hata katika maeneo ya mashambani zaidi ya nchi. Akizungumza pia katika ziara hiyo, Bw Raymond Ochieng Ouma, Katibu wa Ukuzaji wa Vijana alisema Idara ya Masuala ya Vijana na Sanaa itatumia muundo msingi mkubwa wa KNLS kote nchini kufikia watoto na vijana katika kaunti zote 47 kwa kufanya sehemu za maktaba kuwa za dijitali enzi hizi za tekinolojia ya habari na dijitali.

# Kituo cha utafiti chaunda choo cha kupiga jeki nyumba nafuu

ENDELEA KUTOKA UK 1

nana na bakuli ambacho hutumiwa na jamii wa Wasamburu kuchimba mashimo katika ardhi ambayo walifunika baada ya kwenda haja," duru zilisema.

Utengenezaji wa kauri ya choo ya Ngisi unalenga kutatua shida ya viwanda, afya kwa wote na pia kuchochea utengenezaji na kutoa nafasi bora za ajira.

"Utengenezaji wa kauri ya choo unafungama na ajenda ya serikali ya nyumba nafuu, kuunda nafasi za ajira kwa maelfu ya vijana na pia kukuza uchumi.



Choo cha Ngisi kwenye maonyesho ya wiki ya huduma kwa umma 2022 katika KICC, Nairobi.

Vile vile, uvumbuzi huo unatia nguvu mpango wa Nunua Kenya Jenga Kenya kwa kuongeza ushindani na matumizi ya bidhaa zinazozalishwa nchini na huduma kuchochea uzalishaji humu nchini na kuinua viwanda ambavyo ni sehemu muhimu ya Mwongozo wa Uchumi wa Ruwaza ya 2030.

"Kuna ukosefu wa vyombo vya ujenzi vya kauri Kenya na hii inahitaji kushirikiana kwa wadau katika sekta hii. KBRC ilishirikisha SAJ Ceramics, Kazuri Beads na Taasisi ya Utafiti wa Viwanda Kenya (KIRDI) katika mchakato wa utafiti na utengenezaji," duru zilisema.

Bidhaa hiyo imeonyeshwa katika majukwaa kadhaa kama vile Wiki ya Ubunifu ya Nairobi(NIW), Wiki ya Maonyesho ya Utumishi wa Umma, Maonyesho ya Biashara ya Mombasa ya 2022 na katika jamii ya Mukurwe-ini ambako udongo unatoka. Ubunifu huo umezaa Mkataba wa Maelewano (MOU) kati ya (KIRDI) na jamii ya Mukurwe-ini ili kuendeleza uchimbaji wa udongo na pia kunufaisha jamii ya eneo hilo, duru ziliongeza.

MOU hiyo itahakikisha jamii inapata bei nzuri na kuongeza thamani bidhaa wanazotengeneza.


## USAID AMPATH Uzima

Simu: (+254)532033471/2 | Postal Address: P.O. Box 4606-30100, Eldoret, Kenya | B/Pepe: info@usaidampathuzima.or.ke

## TANGAZO LA ZABUNI

USAID AMPATH UZIMA, Mpango unaosimamiwa na Hospitali ya Mafunzo na Rufaa ya Moi (MTRH) na kufadhiliwa na USAID inaalika zabuni zilizofungwa kwa yaliyoorodheshwa hapa chini.

**ZABUNI ZA WAZI KITAIFA**

| No. | NAMBARI YA ZABUNI | MAELEZO YA ZABUNI | UHITIMU | KUFUNGA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | MTRH/T/075/2022-2023 | Utoaji wa Huduma za Mikutano na Ukarimu. | Wazi | Aprili 20, 2023 |
| 2. | MTRH/T/099/2022-2022 | Usambazaj na Uwasilishaji wa Miundo ya Kuiga. | Wazi | Aprili 20, 2023 |
| 3. | MTRH/T/112/2022-2023 | Utoaji wa Tikiti za Ndege na Huduma za Usafiri. | Wazi | Aprili 20, 2023 |

Seti kamili ya hati za Zabuni zitapatikana na Wazabuni wanaovutiwa bila malipo kutoka kwa tovuti rasmi ya MTRH: www.mtrh.go.ke ya zabuni ya serikali: https/supplier.treasury.go.ke.

Zabuni katika bahasha zilizofungwa na kuandikwa nambari ya Zabuni (**iliyokolea**) kwenye kona ya juu kulia lakini bila viashiria vya jina la Mzabuni zinapaswa kuwekwa kwenye Kisanduku cha Zabuni "A", kilicho kwenye Orofa ya Chini, Kituo cha Saratani cha Chandaria au Kutumwa kwa

**Afisa Mkuu Mtendaji**
**Hospitali ya Mafunzo na Rufaa ya Moi**
**P.O. Box 3-30100 ELDORET**

Ili kupokelewa mnamo au kabla ya **Ijumaa tarehe 20 Aprili 2023 saa 10.30 asubuhi**. Zabuni zitafunguliwa hadharani mara baada ya hapo mbele ya Wazabuni au wawakilishi wao watakaoamua kuhudhuria **Kituo cha AMPATH Orofa ya 1 Ukumbi wa ATI Chumba118.**
Zabuni zilizochelewa hazitakubaliwa hata hivyo zitarejeshwa zikiwa hazijafunguliwa.

Makampuni yanayomilikiwa na Vijana, Wanawake na Watu Wenye Ulemavu yanahimizwa kushiriki.

Maswali yote kuhusu zabuni hii yaelekezwe kwa Meneja wa Mfumo wa Usambazaji-USAID AMPATH Uzima

**AFISA MKUU MTENDAJI**
**HOSPITALI YA MAFUNZO NA RUFAA YA MOI**

KENYA VISION 2030



KNBS KENYA NATIONAL BUREAU OF STATISTICS *Keeping you informed*

## SHIRIKA LA KUKUSANYA TAKWIMU KENYA

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Shirika la Kukusanya Takwimu Kenya (KNBS) ni Shirika la Serikali lililoanzishwa chini ya Sheria ya Takwimu (2006). Ni shirika kuu la Serikali lenye jukumu la kukusanya, kuchambua, kuchapisha na kusambaza taarifa rasmi za Takwimu na ulinzi wake. Pia linasimamia uratibu, Usimamizi na uendelezaji wa programu ndani ya Mfumo wa Kitaifa wa Takwimu (NSS).

Shirika la Kukusanya Takwimu Kenya linakaribisha maombi kutoka kwa watu waliohitimu na wenye uzoefu na vyeti bora kujaza nafasi zifuatazo:-

| Jina la Kazi | KNBS | Nambari ya Marejeleo | Idadi | Mfumo wa Uajiri |
|---|---|---|---|---|
| Meneja Msaidizi, Usimamizi wa Rekodi | KNBS Level 5 | KNBS/AMRM/6/2023 | 1 | Ya Kudumu na yenye Pensheni |
| Msaidizi wa Usimamizi wa Rekodi | KNBS Level 8 | KNBS/RMA/7/2023 | 1 | Ya Kudumu na yenye Pensheni |

Maelezo zaidi kuhusu nafasi hizo yatapatikana kwenye tovuti ya KNBS www.knbs.or.ke.

Waombaji wanapaswa kujaza na kuwasilisha nakala ngumu za fomu ya maombi ya ajira yenye Na. KNBS/F/93/29, ambayo inapatikana kwenye tovuti ya KNBS www.knbs.or.ke ikiandamana na nakala za vyeti vya masomo, kitaaluma na vingine muhimu, nakala na ushuhuda. Nambari ya marejeleo ya nafasi iliyoombwa inapaswa kuandikwa vizuri kwenye bahasha na kutumwa kwa:

**Mkurugenzi Mkuu;**
**Shirika la Kukusanya Takwimu Kenya**
**P. O. Box 30266 - 00100**
**Real Towers, Upper Hill, Orofa ya 4**
**Hospital Road**
**NAIROBI**

Maombi lazima yapokewe kabla ya tarehe **31 Machi 2023** na tutawasiliana tu na waombaji watakaoorodheshwa.

**SHIRIKA LA KUKUSANYA TAKWIMUPIA NI MWAJIRI ANAYETOA NAFASI SAWA YA UAJIRI.**

Kenya National Bureau of Statistics is ISO 9001:2015 Certified

KENYA VISION 2030

Funika mdomo unapopiga chafya
20 SEC Nawa mikono na sabuni/ Sanitaiza
Jitenge na walio na virusi
Usiguse macho, pua au mdomo na mikono michafu
Pika nyama na mayai ziive. Usile chakula kibichi
Hakikisha maeneo yote ni safi
KOMESHA COVID-19



# Serikali kubadilisha chakula cha msaada na suluhisho la kudumu–PS

**NA ERICK KYALO(KNA)**

Serikali inatafuta njia za kubadilisha sera zake na mbinu kuelekea usimamizi wa ukame nchini kuwa na suluhisho la kudumu la ukame wa kila mara nchini.

Katibu wa Idara ya Serikali ya Maeneo Kame na Nusu Kame Dkt Idris Dokota alisema kwamba serikali haiko tayari itaendelea kusambaza chakula cha msaada na maji mwaka nenda mwaka rudi na mipango thabiti inafaa kufanywa ili sera nzuri ziundwe kusaidia watu wakati wa misimu ya kiangazi.

Katibu ambaye alikuwa akizungumza katika shule ya msingi ya Dukanotu kaunti ya Tana River katika zoezi la kusambaza chakula cha msaada alisema kwamba serikali itawekeza katika miundomsingi ya maji kwa njia bunifu za kukusanya maji ya mvua, kujenga mabwawa makubwa na kuchimba visima.



Dkt Idris Dokota, Katibu wa Idara ya Serikali ya Maeneo Kame

"Kile ambacho tumekuwa tukifanya ni kukabili dharura, ambayo ni hatua ya muda mfupi, huku ukame ukiwa nasi kwa miaka mingi. Serikali itatafuta njia za kukabiliana na ukame ili tusiwe tukikabili dharura,"Dokota alisema.

"Shida yetu kubwa imekuwa ni ukosefu wa maji. Tukitatua shida ya maji, tutakuwa tumetatua asilimia 60 ya matatizo yetu ya kiuchumi yanayokabili watu wetu," alisema.

Katibu alisema kwamba serikali itasambaza magunia 3,600 ya mchele na magunia 2,000 ya maharagwe kwa watu wote walioathiriwa katika kaunti ndogo zote za Tana River na akaongeza kuwa mpango wa lishe shuleni utaanzishwa ili kuhakikisha watoto wote wanaopaswa kuwa shuleni wanabaki shuleni. Kaunti ya Tana River Ina watu 158,000 wanaohitaji chakula cha msaada huku kiwango cha utapia mlo miongoni mwa watoto kikiwa asilimia 25.

**2000**

**Magunia ya maharagwe yatakayosambazwa Tana**

Naibu Gavana wa kaunti hiyo Mahat Loka, kwa upande wake alisema kwamba serikali inasadiana kwa karibu na taasisi zingine za serikali na mashirika yasiyo ya Serikali kusaidia familia masikini na kupunguza njaa miongoni mwa watu.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na mbunge wa Bura Yakub Adow, Kamishna wa Kaunti Thomas Sankei, Mshirikishi wa Mamlaka ya Taifa ya Kusimamia Ukame kaunti ya Tana River Abdi Musa miongoni mwa wengine. Mapema wiki hii, Waziri wa Ulinzi Aden Duale alisema kwamba kufikia sasa serikali imetumia Sh13 bilioni kununua na kusambaza chakula cha msaada kwa Wakenya ambao wameathiriwa na ukame na ambao wanahitaji chakula cha msaada. Kaunti ambazo ziko katika awamu hatari ni Kilifi, Mandera Marsabit Samburu, Turkana Wajir, Isiolo, Kitui, na Kajiado, huku kaunti 13 za Garissa, Lamu, Narok, Tana River, Makueni, Tharaka Nithi, Baringo, Laikipia, Meru, Taita Taveta, Pokot Magharibi, Maghari na Kwale zikiwa katika awamu ya kuelekea kukumbwa na hatari ya ukame.

# Balozi asifu urafiki wa muda mrefu kati ya Kenya na Japan

**NA EMMANUEL MASHA(KNA)**

Balozi wa Japan Kenya, Ken Okaniwa, amesifu urafiki wa miaka mingi kati ya Kenya na nchi yake na akaeleza matumaini kwamba utaendelea hasa katika uinuaji wa shughuli za Uchumi wa Baharini na kawi salama.

Balozi Okinawa alisema kwamba Kenya na Japan zimekuwa marafiki kwa karibu miaka 60, ambayo alisema umewezesha nchi yake kusaidia kujenga miradi kadhaa ya miundomsingi miongoni mwake Daraja la Sabaki na Kilifi."Tunataka kuinua biashara ya pande mbili na kubadilishanana watu kwa watu kwa sababu ya urafiki huu," akasema Bw Okaniwa katika kiwanda cha kutengeneza meli cha Captain Andy, Watamu, kaunti ndogo ya Malindi. Kampuni ya kutengeneza meli ya Captain Andy ni mojawapo ya kampuni kubwa za kutengeneza na kuuza mashua za uvuvi katika bahari kuu na uchukuzi Afrika Mashariki na ajenti wa humu nchini wa kampuni ya Japan ya YAMAHA Motor Corporation Limited. Ili Kenya iweze kunufaika na rasilmali zote katika bahari, inahitaji kuinua shughuli katika bahari kama uvuvi na uchukuzi wa baharini miongoni mwa mengine," akasema balozi.

Alihimiza Kenya kuunga shughuli za kampuni hiyo ya kutengeneza mashua ambayo alisema imeajiri wakazi 170 na kuchangia pakubwa uchumi wa eneo hilo kupitia kuunda nafasi za ajira, kuwajibikia jamii na ulipaji ushuru.

"Tunapenda Kenya kwa sababu tuko na urafiki wa miaka 60 na ushirikiano. Tumejenga Daraja la Sabaki na daraja zingine tatu Kilifi na Mombasa na tunataka kuinua biashara ya pande mbili na pia kubadilishana watu kwa sababu ya urafiki huu," akasema.

REPUBLIC OF KENYA

KCAA
efficiently managing air safety

## Mamlaka ya Kusimamia Safari za Ndege

## TANGAZO LA ZABUNI

Mamlaka ya Kusimamia Safari za Ndege Kenya inakaribisha zabuni zilizofungwa kutoka kwa kampuni zinazovutiwa na zinazostahiki kwa Zabuni Wazi Kitaifa Zifuatazo.

| NA | NAMBARI YA ZABUNI | MAELEZO/KICHWA CHA ZABUNI | KUZURU ENEO | UHITIMU | KUFUNGA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | KCAA/054/2022-2023 | Kuhuisha leseni za Microsoft 365 kwa muda wa miaka mitatu (3). | N/A | Mwananchi | Jumatano, Aprili 5, 2023 saa 11:00 asubuhi |
| 2. | KCAA/055/2022-2023 | Uonyeshaji Nia (EOI) kwa utoaji wa Huduma za Ushauri za Usanifu, Utayarishaji wa Hati za Zabuni na Usimamizi wa Ujenzi wa Vyumba vya Madarasa na Ofisi katika Kitalu cha Uhandisi cha EASA | Jumatatu, Machi 27, 2023 saa11asubuhi hadi Saa 1 mchana katika EASA | Mwananchi | |
| 3. | KCAA/056/2022-2023 | Utoaji wa Huduma za Ushauri ili Kufanya Uhakiki wa Mali za Kudumu | N/A | Mwananchi | |
| 4. | KCAA/058/2022-2023 | Usambazaji, Utoaji na Ufungaji wa Mfumo wa Mitihani wa AVSEC | N/A | Mwananchi | |

Kwa maelezo zaidi kuhusu zabuni mbalimbali, wazabuni wanaweza kutazama na kupakua hati za zabuni kutoka tovuti ya KCAA: www.kcaa.or.ke au Tovuti ya Taarifa ya Ununuzi wa Umma, www.tenders.go.ke na kutuma mara moja taarifa zao ili kunakiliwa na kwa madhumuni ya kupokea ufafanuzi wowote zaidi wa zabuni na/au nyongeza kwa procurement@kcaa.or.ke

Nyaraka zilizokamilishwa za zabuni zinapaswa kuambatanishwa katika bahasha zilizofungwa zilizoandikwa nambari ya kumbukumbu ya zabuni na kuwekwa kwenye Sanduku la Zabuni kwenye Orofa ya Chini, **Mamlaka ya Kusimamia Safari za Ndege Kenya, Jumba la Aviation, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta,** au kutumwa kwa:

**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Kusimamia Safari za Ndege Kenya,**
**P.O Box 30163-00100, Nairobi**

Ili kupokelewa kabla ya tarehe na wakati ulioonyeshwa dhidi ya zabuni husika ifikapo **saa 11:00 asubuhi.**
Zabuni zitafunguliwa mara moja baada ya hapo mbele ya Wagombea au wawakilishi wao watakaoamua kuhudhuria katika Ukumbi wa KCAA.

**Meneja wa Ununuzi**
**KWA: MKURUGENZI MKUU**

KENYA VISION 2030

ENGINEERS BOARD OF KENYA
Enhancing Professionalism

## UKUZAJI KITAALUMA UNAOENDELEA KWA WAHANDISI SHUGHULI ZA MWAKA 2023

Bodi ya Wahandisi Kenya ni chombo cha kisheria kilichoanzishwa chini ya Kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Wahandisi 2011. Bodi ina jukumu la usajili wa wahandisi na makampuni ya uhandisi, udhibiti wa huduma za kitaaluma za uhandisi, kuweka viwango, maendeleo, na mazoezi ya jumla ya uhandisi.

Kifungu cha 7(1)(q) cha Sheria ya Wahandisi ya 2011 kinaiagiza Bodi ***"kupanga, kupanga na kusimamia mafunzo endelevu ya kitaaluma na maendeleo ya wahandisi."*** Bodi inaendesha Mpango wa Kukuza Taaluma ambao unalenga kuwasaidia wahandisi kusasishwa na mitindo na maendeleo ya kisasa katika tasnia, kuboresha ujuzi wao, na ujuzi wa hatimaye kuendeleza taaluma zao.

Bodi imebuni kalenda ya shughuli za CPD kwa kalenda ya 2023 yenye aina mbalimbali za kozi, warsha, semina na makongamano yaliyoundwa ili kuwafunza wahandisi kuhusu mitindo na maendeleo ya kisasa katika mazingira yaliyojengwa. Kalenda huangazia matukio kutoka kwa Bodi pamoja na mashirika yanayoaminika katika sekta hii, ikijumuisha vyama vya kitaaluma, na watoa mafunzo walioidhinishwa na Bodi. Wahandisi wanaalikwa kuchagua programu kutoka kwa mada anuwai, kutoka kwa mafunzo na maeneo mahususi ya mafunzo hadi teknolojia ya uhandisi, kandarasi na usimamizi wa mradi pamoja na maswala yanayoibuka katika uhandisi na maeneo mengine muhimu.

Kalenda ya 2023 ya shughuli za CPD inapatikana katika tovuti ya Bodi katika www.ebk.go.ke. Wahandisi wanashauriwa kutembelea tovuti ya Bodi ili kupata kalenda na orodha ya taasisi zilizoidhinishwa na Bodi kutoa mafunzo ya CPD.

**Msajili/Afisa Mkuu Mtendaji**
**Bodi ya Wahandisi Kenya**
**Fortis Suites, Orofa ya 9, Hospital Road, Upper Hill**
**P.O Box 30324-00100 Nairobi, Kenya**

KENYA VISION 2030

“ Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa”

HOMA · KIKOHOZI · KUSHINDWA KUPUMUA · MAUMIVU KOONI · KUUMWA NA KICHWA

# Afueni kwa wakazi 10,000 wa Makueni bwawa la Ndukuma likifanyiwa ukarabati



**NA PATRICK NYAKUNDI NA RONALD RONO(KNA).**

Wakazi zaidi ya 10,000 kutoka wadi ya Kikumini/Muvau kaunti ndogo ya Makueni watanufaika na kuchimbuliwa kwa bwawa la Ndukuma. Bwawa hilo linakarabatiwa na serikali ya kaunti ya Makueni kwa gharama ya Sh 50 milioni.

Gavana wa Makueni Mutula Kilonzo Junior alisema kwamba bwawa hilo lililo na uwezo wa kuhifadhi lita milioni mia saba za maji litahudumia vijiji 10 katika eneo hilo na mji wa Wote baada ya kukamilika mwishoni mwa mwezi.

“Baada ya kukamilika kwa mradi huu katika muda wa wiki moja au mbili zijazo, bwawa litakuwa na lita milioni mia saba za maji ambayo yatahudumia wakazi wa vijiji 10 na mji wa karibu wa Wote,” alisema Mutula baada ya kufungua bwawa hilo Jumatano. Vijiji hivyo kumi ni Kaseve, Nthembe, Mandoi Miteveni, Wendo, Munyuni, Nzaai, Kiatine na Mumbuni kaunti ndogo ya Makueni.

> Tuna vituo 16 vya maji na tumekodisha vifaa vya ziada,” - Kieti

Gavana alisema kwamba wameanza awamu ya pili ambayo watajenga kiwanda cha kuwekea maji dawa na tanki la kuhifadhi maji ambalo litawezesha wakazi kutumia nyumbani na kwa unyunyuzaji mdogo. Wakati huo huo, mkuu wa kaunti aliomba serikali ya kitaifa kufadhili serikali ya kaunti kujenga mabwawa badala ya kutoa chakula cha msaada. Alisema hatua hiyo itapiga jeki utoshelevu wa chakula katika kaunti kwa kuwa wakulima wa mashamba madogo watatumia maji hayo kunyunyiza mashamba yao na hivyo basi kuimarisha uzalishaji wa chakula na kuacha kutegemea chakula ghali za misaada. “Hii ndiyo suluhu ya utoshelevu wa chakula, serikali za kaunti ziko na uwezo wa kufanya miradi hii kwa gharama ya chini ikilinganishwa na serikali ya kitaifa,” alisema.

Akizungumza katika hafla hiyo, Waziri wa Maji na Usafi wa kaunti Mhandisi John Kasyoki Kieti alisema kazi ya ukarabati ilihusisha kuchimbua mchanga uliokusanyika kwa muda, kutia nguvu ukuta wa bwawa kuepuka kuvuja.

Kieti pia alifichua kwamba bwawa hilo litakuwa na zingine ndogo kuzuia mchanga na kujenga ya na kupanda miti katika ekari 58. “Tuko na vitua 16 vya kuchota maji. Usambazaji wa maji unatumia pampu, nguvu za sola, mabomba ya kujengwa na mafundi na matangi ya maji,” alisema Mhandisi Kieti. Alifichua kwamba walikodisha vifaa zaidi kutoka kwa Shirika la Vijana wa Huduma kwa Taifa (NYS) kusaidia vifaa vya idara na kuharakisha kazi.

---

EACC

## ETHICS AND ANTI-CORRUPTION COMMISSION

**OUR MISSION**

***“To promote integrity and combat corruption through law enforcement, prevention and education.”***

## VACANCIES

The Ethics and Anti-Corruption Commission (EACC) is established under Section 3 of the Ethics and Anti-Corruption Act, No. 22 of 2011, pursuant to Article 79 of the Constitution of Kenya. The mandate of the Commission is to combat and prevent corruption and economic crime in Kenya through law enforcement, preventive measures, public education and promotion of standards and best practices of integrity, ethics and anti-corruption.

The Commission invites applications from suitably qualified persons to fill the following positions:

| S/No | Position | EACC Grade | Vacancy Ref. No. | Number of Posts |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Senior Security Officer | 6 | EACC/CSS/SSO/9 | 1 |
| 2 | Investigation Officer II – Lawyer | 8 | EACC/INV/IOIIL/1 | 1 |
| 3 | Investigation Officer II – Intelligence | 8 | EACC/INV/IOIII/2 | 1 |
| 4 | Education Officer II | 8 | EACC/PS/EOII/3 | 1 |
| 5 | Legal Officer II | 8 | EACC/FSC/LOII/6 | 2 |
| 6 | Accountant II | 8 | EACC/FP/AII/4 | 1 |
| 7 | Accounts Assistant I | 9 | EACC/F&P/AAI/5 | 1 |
| 8 | Paralegal Clerk II | 10 | EACC/FSC/PLCII/8 | 1 |
| 9 | Administrative Secretary II | 10 | EACC/CSS/ASII/10 | 1 |
| 10 | Driver II | 11 | EACC/CSS/DII/11 | 3 |
| 11 | Office Assistant III | 12 | EACC/CSS/OAIII/12 | 2 |
| | Total | | | 15 |

Interested candidates should complete ***EACC Form 1*** online from **https://jobs.integrity.go.ke** and attach copies of ID, CV, academic/ professional certificates and testimonials. The details of the job descriptions and requirements are provided on our website **www.eacc.go.ke.**

All applications must be made online and will be acknowledged via an email. Only shortlisted candidates will be invited for interview.

The applications should be received **not later than Thursday, 30th March, 2023 at 5.00 pm.**

***EACC is an equal opportunity employer. Canvassing will lead to automatic disqualification.***

KENYA VISION 2030

---

KNTC
Kenya National Trading Corporation Ltd.

## TANGAZO LA ZABUNI

Shirika la Kitaifa la Kusimamia Biashara Kenya (KNTC) ni Shirika la Serikali katika Wizara ya Uwekezaji, Biashara na Viwanda ambalo jukumu lake ni kutoa huduma za wakala wa Ununuzi kwa Serikali, kukuza biashara ya jumla na rejareja kupitia usambazaji wa bidhaa muhimu nchini na bidhaa kuu ikiwa ni pamoja na Mbolea, Mpunga, Zana za Shamba Mbalimbali, Vifaa vya Kiufundi kati ya vifaa vingine vya jumla. KNTC pia hutoa nafasi ya Biashara na huduma kwa umma kwa ujumla kando na kusaidia SME nchini kupitia kutafuta masoko ya ndani na nje ya bidhaa zao.

Shirika linakaribisha maombi ya zabuni Wazi/usajili wa wasambazaji kutoka kwa wazabuni wanaovutiwa na wanaostahiki kwa bidhaa, huduma na kazi zifuatazo kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2023/2024 na 2024/2025.

**A. Uhitimu wa awali/ Usajili wa Wasambazaji**

| | Nambari ya Zabuni | Maelezo |
|---|---|---|
| 1. | KNTC/020/2023-2025 | Uhitimu wa awali/Usajili wa Wasambazaji kwa Ugavi/Utoaji wa bidhaa, kazi na huduma kwa kipindi cha miaka ya kifedha 2023/2024 hadi 2024/2025. |

**B. Zabuni**

| | Nambari ya Zabuni | Maelezo ya Zabuni | Uhitimu |
|---|---|---|---|
| 1. | KNTC / TENDER/MEDICAL INSURANCE/ 021-2023-2024 | Utoaji bima ya matibabu kwa Wakurugenzi na wafanyikazi | Madalali/Mawakala |
| 2. | KNTC/TENDER/GROUPLIFE/022/ 2023-2024 | Utoaji Huduma za Bima ya Maisha ya Kundi kwa Wafanyakazi | Madalali/Mawakala |
| 3. | KNTC/TENDER/GENERAL INSURANCE/ 023/2023-2024 | Utoaji wa huduma za Bima ya Jumla | Madalali/Mawakala |

Nyaraka za zabuni zilizo na mahitaji ya kina zinaweza kupakuliwa bila malipo kutoka kwa tovuti yetu **www.kntc.co.ke** na tovuti ya maelezo ya manunuzi ya umma (PPIP) **www.tenders.go.ke**

Ufafanuzi na/au marekebisho yote yatachapishwa katika tovuti ya KNTC na wazabuni wanatakiwa kuangalia mara kwa mara nyongeza au marekebisho yoyote katika kipindi cha zabuni kabla ya tarehe ya kufungwa.

Nyaraka zilizokamilishwa za Zabuni lazima ziwasilishwe katika bahasha iliyofungwa na ilyoandikwa kwa **Mfano-'NAMBARI YA ZABUNI:** na kuwekwa kwenye Sanduku la Zabuni katika Afisi Kuu ya KNTC, Orofa ya Chini, Yarrow Road Complex, Off Nanyuki Road, Industrial Area, Nairobi mnamo au kabla ya tarehe **4 Aprili, 2023 saa 10:00 asubuhi**, na itiumwe kwa:

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Shirika la Kitaifa la Kusimamia Biashara Kenya**
**P.O. Box 30587-00100**
**NAIROBI**

NB: Nakala ngumu zinaweza kununuliwa kwa kshs 1000.00 kutoka ofisi yetu kuu.

**Zabuni Zilizochelewa HAZITAKUBALIWA**

KENYA VISION 2030






REPUBLIC OF KENYA

Kenya Power

## MWALIKO WA KIKAO CHA WASAMBAZAJI (YW&PWD)

Kenya Power inaalika kampuni zinazomilikiwa na Vijana, Wanawake na Watu Wenye Ulemavu (YW&PWD) kwa kongamano la nusu siku la uhamasishaji Jumanne tarehe 28 Machi 2023 kuanzia saa 8.00 asubuhi hadi 12.30 mchana katika Stima Club, Ruaraka – kando ya Barabara ya Thika, itakayoendeshwa na Kitengo cha Usambazaji.
Kila kampuni inaruhusiwa kutuma mwakilishi mmoja tu.

| | |
|---|---|
| **Hadhira Lengwa:** | Makundi Maalum - Vijana, Wanawake na Watu Wenye Ulemavu |
| **Maudhui:** | Uhamasishaji kuhusu fursa za ununuzi katika KPLC chini ya Upendeleo na Uhifadhi. Upeo huo utajumuisha muhtasari wa hati za zabuni za KPLC, vidokezo vya jinsi ya kuweka zabuni zilizofaulu, kandarasi za ununuzi na Kanuni za Maadili za Wasambazaji. |

Mahudhurio ya mkutano yatahusu tu wale ambao wameonyesha nia ya kuhudhuria kwa barua-pepe kwa srmtraining@kplc.co.ke. Unaombwa kujiandikisha kabla ya 4.00 jioni Ijumaa, Machi 24, 2023 kwa mkutano huo.

Vipindi vya ziada vinaweza kupangwa kulingana na mahitaji.

**Kumbuka: Vipindi hivi vinakusudiwa tu kuhamasisha na havikusudiwi au havikusudiwi kwa vyovyote kuwapa washiriki manufaa yoyote yasiyofaa kuhusu Zabuni za Kenya Power.**

**www.kplc.co.ke**

DIAL *977# | Access Kenya Power services fast and easy
www.kplc.co.ke @Customercare.kplc.co.ke Kenya Power @KenyaPower 97771 0703-070 707, 0732-170 170

---

REPUBLIC OF KENYA

## KENYA PIPELINE COMPANY LIMITED

***Africa's Premier Oil & Gas Company***

KPC

KENPIPE PLAZA,
SEKONDI ROAD,
OFF NANYUKI ROAD,
INDUSTRIAL AREA,
NAIROBI, KENYA.
P.O.Box 73442 - 00200,
TELEPHONE: 254-20-2606500-4
MOBILE: 0722 207 678/9
0734 333 217/219/234/226
E-mail: Info@kpc.co.ke

## KUFUTILIWA MBALI KWA TENDA

Kenya Pipeline Company Limited ingependa kufahamisha wote waliotuma maombi kuwa tenda hii imefutilwa mbali

| NO. | NAMBARI NA MAELEZO YA TENDA | TAREHE YA KUZURU | SIKU YA MWISHO |
|---|---|---|---|
| | **OPEN NATIONAL TENDER** | | |
| 1. | **KPC/PU/OT-264/ADM/NBI/22-23**<br><br>Tenda ya kukodisha vyumba vya maakuli katika Makao Makuu- Kenpipe Plaza, Plaza PS 25 – Nakuru na PS 28 Kisumu | MAKAO MAKUU NAIROBI<br>01.03.2023<br>08.03.2023<br><br>NAKURU<br>02.03.2023<br>09.03.2023<br><br>KISUMU<br>03.03.2023<br>10.03.2023 | 23-03-2023 |

CANCELLED

**Kaimu. MENEJA MKUU (UNUNUZI)**
**KWA NIABA YA: MKURUGENZI MKUU**

KENYA VISION 2030

---

REPUBLIC OF KENYA

## THE NATIONAL TREASURY AND ECONOMIC PLANNING

## INVITATION TO TENDER

The National Treasury invites sealed Tenders from eligible candidates for the following: -

| S/No | Tender No. | Description | Bid Security (Kshs) | Closing Date | Pre bid conference date |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | TNT/021/2022-2023 | Provision of Management and Operation of National Treasury Gym/ Health Club at the Thirteenth (13TH) Floor of Bima House, Nairobi | 300,000.00 | Wednesday 5th April, 2023 at 11.00 a.m. | Tuesday 28th March, 2023 at 10.00 a.m. |
| 2. | TNT/022/2022-2023 | Provision of Oracle Application Support Licenses | 5,000,000.00 | Friday 7th April, 2023 at 11.00 a.m. | Wednesday 29th March, 2023 at 10.00 a.m. |

A complete set of Tender Documents may be downloaded by interested firms free of charge at **www.treasury.go.ke** or **www.tenders.go.ke** and those who download the document from the website must forward their particulars immediately for recording and any further clarifications and addenda to **procurement@treasury.go.ke**.

A Mandatory Pre-Bid Conference shall be held with the interested Bidders as indicated above at **10.00 a.m.** through video conferencing. Invitations shall be send to all interested tenderers who shall submit their emails to **procurement@treasury.go.ke** before **10.00 a.m.** as indicated above.

Completed Tender Documents, both ***"Original"*** and ***"Copies"***, enclosed in plain sealed envelopes, marked with the relevant Tender Number and Title shall be addressed to:

**The Principal Secretary,**
**The National Treasury,**
**P. O. Box 30007 – 00100,**
**Nairobi, Kenya**

and be deposited in the Tender Box provided at the **Treasury Building, 6th Floor, Harambee Avenue, Nairobi,** so as to be received on or before the closing dates indicated above.

Bids shall be accompanied by an Original Bid Security from a **Reputable Bank in Kenya valid for 30 days beyond the Tender Validity period as indicated above.**

All Bid Documents must be sequentially serialized / paginated.

Tenders will be opened immediately thereafter in the presence of the tenderers or their representatives who choose to attend the opening at **The National Treasury, Treasury Building, Harambee Avenue, Nairobi, 6th Floor, Conference Room No. 603 on the indicated closing dates.**

**HEAD, SUPPLY CHAIN MANAGEMENT SERVICES.**
**FOR: PRINCIPAL SECRETARY / NATIONAL TREASURY**

KENYA VISION 2030

---

KENYA RE

## KENYA REINSURANCE CORPORATION LTD

## INVITATION TO TENDER

Kenya Reinsurance Corporation Limited invites sealed tenders from eligible candidates for the following items as detailed in the tender document:

| TENDER NO: | DESCRIPTION | TENDER SECURITY (KSHS.) | TENDER SUBMISSION FORMAT | ELIGIBILITY |
|---|---|---|---|---|
| **INVITATION TO NATIONAL TENDER** | | | | |
| KRC/1999/2023/054 | SUPPLY OF SEVENTY (70) LAPTOPS | TENDER SECURING DECLARATION FORM SIGNED AND STAMPED | COMBINED TECHNICAL AND FINANCIAL PROPOSALS | RESERVED FOR YOUTH |
| KRC/2025/2023/051 | REQUEST FOR PROPOSAL FOR CONSULTANCY FOR IT CAPABILITY AND MATURITY ASSESSMENT | KSHS. 95,000.00 | SEPARATE TECHNICAL AND FINANCIAL PROPOSALS | OPEN |

Prospective bidders may download the tender documents from the Kenya Reinsurance Corporation Limited website **www.kenyare.co.ke** free of charge or Public Procurement Portal **www.tenders.go.ke.** Tender documents in plain sealed envelopes clearly bearing the correct **tender number** and name should be deposited in the Tender Box located on the 16th floor of Reinsurance Plaza Aga Khan Walk NAIROBI or be sent to:-

**Managing Director**
**Kenya Reinsurance Corporation Limited**
**Reinsurance Plaza, Nairobi**
**Aga Khan Walk**
**P.O. Box 30271 - 00100**
**NAIROBI**

To be received on **4TH APRIL 2023 AT 10.00 A.M.** Tenders will be opened the same day and time at Reinsurance Plaza, Nairobi Aga khan Walk on the 17th floor in the presence of bidders or their representative who choose to attend. Tenders that are delivered after the submission deadline will be rejected.

Prices quoted **MUST** be expressed in the currency detailed in the invitation to tender inclusive of Kenyan Government taxes (VAT, WITHHOLDING TAX) and should remain valid for a period of **120 days** from the date of closing of the tender.

Bidders who download the tender documents from the Corporation website or the Public Procurement Portal **MUST** forward their particulars immediately via email to **procurement@kenyare.co.ke.** This is for record and any further tender clarifications and addendum where necessary. The particulars should include: Name of Firm, Postal Address, Telephone Number, Email Address, Tender Number and Tender Name. The said e-mail may be used for clarification.

Any canvassing or giving of false information will lead to automatic disqualification.

KENYA VISION 2030 *Kenya Re is ISO 9001:2015 and ISO 27001:2013 Certified*

“ Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa”
HOMA · KIKOHOZI · KUSHINDWA KUPUMUA · MAUMIVU KOONI · KUUMWA NA KICHWA

# Kenya sasa Korea Kusini kwenye ushirikiano kukuza sekta ya ICT

**NA EVALYNE GITHINJI (PCO)**

Kenya na Korea Kusini zimezindua ushirikiano wa maendeleo wa sekta ya ICT unaoitwa “Mpango wa Ushirikiano wa Ubunifu wa Uchumi”(EIPP) ambao uko katika mwaka wake wa pili wa utekelezaji.

Akizungumza katika uzinduzi wa ushirikiano huo katika hoteli ya Nairobi, Waziri wa Habari Eliud Owalo alisema kwamba EIPP itaharakisha utekelezaji wa miradi ya miundomsingi muhimu ya ICT, na ustawi wa miji hasa katika Konza Technopolis.

“Uzinduzi huu, unafuatia kufaulu kwa utekelezaji wa miradi kwa mwaka mmoja chini ya mpango huo mwaka jana baada ya kutia saini MOU jijini Nairobi.

> Uzinduzi huu unafuatia utekelezaji uliofanikiwa wa miradi ya awamu ya kwanza -Owalo

"Mwaka mmoja wa miradi ulihusu miradi mitatu inayohusiana na maendeleo ya jiji la Konza Smart City. Hii ilikuwa mikakati ya jiji la kitekinolojia, Kituo cha pamoja cha Usimamizi wa Konza Technopolis na Usafiri wa Kisasa katika Konza City,” alisema Owalo.

Alisema kwamba miradi zaidi imeidhinishwa kutekelezwa katika mwaka wa pili wa mpango wa maendeleo miongoni mwao, utafiti wa ufaafu wa mfumo wa Uchukuzi wa (ITS) na Kituo cha Pamoja cha Uelekezi (ICC).

Miradi mingine, alisema waziri, ni kuanzishwa kwa mfumo wa mazingira katika Konza Technopolis kwa uchukuzi wa kisasa na maendeleo ya mtandao wa uchukuzi wa Konza-Nairobi.



Waziri Eliud Owalo

Kwa mara nyingine, Owalo alishukuru kwa usaidizi kutoka Korea Kusini ambao umewezesha Kenya kuanzisha miradi kadhaa muhimu ya ICT katika Konza Technopolis ambayo iko katika awamu tofauti za utekelezaji.

Baadhi ya miradi inayofadhiliwa na Korea Kusini katika Konza Technopolis ni pamoja na; Taasisi ya Kuendeleza Sayansi na Tekinolojia ya Kenya (KAIST) ambayo iko chini ya ujenzi na Konza Digital Media City.

Mbali na kufadhili miradi ya miundomsingi ya ICT, Waziri Owalo alisema EIPP pia inapata usaidizi kutoka Korea EXIM Bank inayofadhii utafiti wa ufaafu kamili na mpango mkuu wa jiji hilo la kisasa.

“Ninashukuru sana ushirikiano wa Mamlaka ya Maendeleo ya Konza Technopolis (KoTDA) na Shirika la Uwekezaji na Uinuaji wa Biashara la Korea (KOTRA) kwa kutia nguvu uhusiano wa kirafiki kati ya Kenya na Korea kupitia utekelezaji wa miradi hii,” alisema Waziri Owalo.

Kwa upande wake, Meneja Mkurugenzi wa KOTRA Ik Hyun alifurahishwa na kufaulu kwa EIPP katika mwaka wake wa kwanza wa utekelezaji na akaelezea matumaini ya kufaulu siku zijazo.

# Duale asisitiza kujitolea kwa Wizara kuheshimu utawala wa sheria

**NA BOGITA ONGERI, (PCO)**

Wizara ya Ulinzi itawajibika kila wakati wa Amiri Jeshi Mkuu wa Jeshi la Ulinzi la Kenya mbali na Bunge kupitia kamati husika za Bunge, Waziri wa Ulinzi, Aden Duale amesema.

Duale alisema kwamba uaminifu kwa Amiri Jeshi Mkuu ni hitaji la kisheria na la lazima kwa KDF.

Waziri alifichua kwamba jeshi limeamriwa na Rais kukarabati shule katika ukandawa Kaskazini Mashariki ambazo ziliharibiwa na majangili na kujenga shule mpya kuwezesha watoto kuendelea na masomo yao kama wenzao walio katika maeneo mengine ya nchi.

Duale alisema haya alipofungua warsha ya siku mbili ya Kamati ya Bunge kuhusu Ulinzi, Ujasusi na Mashauri ya Kigeni na Maafisa wa Ulinzi mjini Mombasa.

Katika warsha hiyo, waziri aliwasilisha operesheni kadhaa ambazo Jeshi la Ulinzi la Kenya (KDF) linatekeleza sehemu tofauti za nchi na nje ya Kenya, na akaongeza kuwa vita dhidi ya ujangili katika Kaskazini mwa Bonde la Ufa vimekuwa na matokeo mazuri katika wiki kadhaa zilizopita.

Warsha hiyo iliyoleta pamoja maafisa wakuu wa wizara ya na jeshi, inalenga kuwafahamisha wanachama wa kamati hiyo kuhusu mambo tofauti ambayo wizara inahusika nayo ndani ya majukumu yake ya kutoa ulinzi na usalama wa mipaka ya Jamhuri.

Duale aliomba kamati, inayosimamiwa na Mbunge wa Belgut kutenga bajeti inayotosha kusaidia mpango wa kuwapa wanajeshi nyumba nzuri na kununulia KDF vifaa vya kisasa kuimarisha uwezo wake.



Waziri wa Ulinzi, Aden Duale

Waziri alisema kwamba jeshi limepiga hatua katika kugatua kambi za jeshi ambazo ziko katika miji mikubwa hadi sehemu za ndani za nchi akisema tishio la usalama kwa wakati huu linatoka maeneo kama hayo. “Tunataka tuwe na kambi za kijeshi Turkana, Marsabit, Mandera, Lamu, Kwale na maeneo mengine ili kuchukua hatua haraka nyakati za tishio,” alisema waziri.

# Anzisheni mikopo inayowezesha vijana zaidi, waziri aambia bodi

**NA MATHEW KANDIE (MYGOV)**

Waziri wa Ushirika na Ustawi wa Biashara ndogo Simon Chelugui amehimiza Bodi mpya ya Hazina ya Maendeleo ya Biashara ya Vijana (YEDF) kupanga mambo yake kwa kuzingatia mikopo na huduma za kusaidia biashara ili kuwezesha vijana.

Chelugui aliambia bodi ya YEDF kujifahamisha kuhusu mabadiliko ya kiuchumi yanayoendelea ulimwenguni huku viwanda na sekta mpya zikiibuka na zingine zikididimia na kuweka huduma zitakazolandana na mazingira ya sasa ya biashara ulimwenguni.

Waziri Chelugui ambaye alikuwa akizungumza alipozindua bodi mpya ya YEDF katika makao makuu ya hazina hiyo alisema: “Katika hali hii, ninatarajia bodi kulenga kubadilisha hazina kwa kupeleka vijana katika maeneo mapya ya biashara, kama ujenzi na pia katika mifumo ya kuongeza thamani katika viwanda vya maziwa, ngozi, mafuta ya kula na viwanda vya pamba”. Waziri alisema kwamba maendeleo ya kitekonojia yanaathiri shughuliza biashara na ujuzi unaohitajika kufaulu na MPANGO wa Kenya Kwanza unasisitiza umuhimu wa mabadiliko ya dijitali kama kiwezeshi muhimu cha ukuaji wa uchumi na maendeleo Kenya. MPANGO huo, Chelugui alisema unaeleza mikakati na mbinu za kuinua mabadiliko ya dijitali Kenya, ikiwemo kuimarisha utoaji wa huduma za serikali kupitia dijitali.



Waziri wa Ushirika na Biashara Ndogo Simon Chelugui

# Kumbatieni unyunyuzaji, Katibu ahimiza wakulima wa kaskazini

**NA ERICK KYALO (KNA)**

Wakulima wanaofuga ng’ombe katika ukanda wa Kaskazini Mashariki wamehimizwa wakumbatie kilimo cha mimea kama chanzo mbadala cha kujikimu kimaisha huku eneo hilo likikumbwa na ukame wa muda mrefu. Katika miaka michache iliyopita hali ya ukame katika eneo hilo imeendelea kuwa mbaya na kusababisha mamilioni ya mifugo kufariki na watu wakikabiliwa na njaa bila njia za mapato. Akizungumza baada ya kutembelea mashamba kadhaa yanayonyunyuziwa maji na kufungua visima katika Habaswein, kaunti ya Wajir, Katibu wa Idara ya Serikali ya Maji na Unyunyuzaji Kiprono Rono alisema eneo hilo linaweza kuzalisha chakula kingi kwa kuwa ardhi ina rotuba kwa sababu haijawahi kulimwa.

Rono alisema serikali inajitahidi kupata chanzo cha maji ya kudumu katika eneo hilo kupitia ujenzi wa mabwawa makubwa na kuchimba visima vinavyotoa maji kwa wingi kufanikisha kilimo cha unyunyuzaji. “Hili ni eneo ambalo tunahitaji maji tu kwa sababu mchanga una rotuba na wakulima hawahitaji mbolea. Wakisaidiwa, wakulima wanaweza kupata chakula cha kutosha cha kutumia na kuuzia maeneo mengine,” alisema Rono.

“Kama serikali ya kitaifa, kupitia Wizara ya Maji na Unyunyuzaji, tutafanya kila tuwezalo kusaidia eneo hili na maeneo mengine ya nchi yaliyo na ardhi ya kutosha na yanahitaji maji tu kuzalisha mimea ya chakula,” aliongeza.



Katibu wa Maji Kiprono Rono ahutubia waandishi habari baada ya kutembelea mashamba yanayonyunyiziwa maji






# Wizara yatafuta usaidizi wa Bunge kuhusu utunzaji wa mazingira

NA NANCY MATHU (PCO)


Waziri wa Mazingira, Soipan Tuya, (kati) akiwa kwenye warsha na maseneta mjini Nakuru.

Wizara ya Mazingira, mabadiliko ya Tabia nchi na Misitu imetoa mapendekezo kadhaa kwa Bunge la Taifa na Seneti kuoanisha ulinzi wa Mazingira na Uchumi nchini.

Kwa muktadha huu, Waziri wa Mazingira, Mabadiliko ya Tabia nchi na Misitu Bi Soipan Tuya anahimiza kamati za bunge zinazohusika na Wizara yake kuchunguza baadhi ya sheria muhimu zinahusu matatizo ya sasa ya mazingira.

" Shida nyingi ambazo tumetambua chini ya Sheria ya sasa ya Ushirikishi wa Usimamizi wa Mazingira (EMCA), Sheria ya Utunzaji na Usimamizi wa Misitu na sheria husika, hasa vizingiti kwa utekelezaji wake zinafaa kushughulikiwa kikamilifu na kutatuliwa katika mapendekezo ya sheria," alisema Waziri huyo.

Akitambua kwamba sheria za mazingira na sera katika miongo mitatu iliyopita zimeafikia mengi, Waziri Soipan alisema kuna haja ya kubadilisha baadhi ya sera na sheria kuwezesha Wizara kufungua nafasi katika sekta husika na pia kuimarisha ushirikishi wa jamii mashinani. Chini ya EMCA, wizara inataka kupitishwa kwa Mswada wa EMCA wa 2022; kuinua kiwango cha Taasisi ya Utafiti wa Misitu Kenya (KEFRI) na Shirika la Minara ya Maji la Kenya (KWTA) ambazo zinahudumu chini ya ilani za sheria, na kufanya Idara ya Utabiri wa Hali ya Hewa Kenya (KMD) kuwa shirika huru.

Masuala mengine aliyowasilisha ni kufungamanisha Mkakati wa Ukaguzi wa Mazingira na EMCA, Sheria za kushughulikia taka ya tairi 2023 na mfumo kazi wa kuidhinisha marufuku ya mifuko ya plasitiki.

Waziri alisema kwamba kuna haja ya kubadilisha Sheria ya Mabadiliko ya Tabia nchi ya 2016 kuwezesha Kenya kunufaika na sekta ya mabilioni ya pesa ya soko la kaboni.

Sekta muhimu zinazotarajiwa kufungua biashara ya kaboni ni misitu, kilimo, kawi, uchukuzi, mashamba katika maeneo kame na nusu kame. Soko hili linatarajiwa kuunda nafasi 300-700 za ajira.

Bi Soipan alionya raia dhidi ya vitendo vya kuharir mazingira akitaja mioto ambayo iliharibu hektari karibu 40,000 za msitu wa Aberdares.

"Tunahitaji kukaza adhabu kwa makosa ya mazingira na misitu kwa kuweka sehemu za kuhamasisha umma," alisema. Katibu wa Idara ya Serikali ya Mazingira Mhandisi Festus K Ngeno aliomba wabunge kubadilisha EMCA, 1999 na kuunga Mswada wa EMCA, 2022 kuwa na haki za watetezi wa mali asili na mazingira, uhalifu wa kuua mazingira, ulinzi wa Misitu maeneo ya Mijini na bustani.

Idara ya Serikali ya Misitu iliomba sera ya kitaifa ya Misitu ya 1968 ibadilishwe. Mapendekezo mengine ni Kanuni na Sheria za Makaa 2023; kuanzishwa kwa Mamlaka vya Kuthibiti Misitu miongoni mwa mengine. Pia waliwasilisha mapendekezo kuhusu Prosopis Juliflora mumea maarufu kama Mathenge ambao ulizua malalamishi kutoka kwa jamii na watetezi wa mazingira wanaotaka uthibitiwe.

# Uwanja wa Michezo wa pili kutumia tekinolojia ya simiti



Shughuli za ujenzi zaendelea katika uwanja wa michezo wa Embu

NA JUSTUS ANZAYA (KNA)

Mwanakandarasi anayekarabati uwanja wa michezo wa Embu utakaoandaa Madaraka Dei mwaka huu amefichua uwanja huo utakuwa wa pili Kenya kutumia tekinolojia ya simiti.

"Hii ni baada ya uwanja wa michezo wa Kirigiti kaunti ya Kiambu," alifichua Sagar Saghani, mwanakandarasi anayekarabati uwanja huo wa michezo.

Alisema kwamba Kenya ni nchi ya kwanza Afrika Mashariki kutumia tekinolojia hiyo katika ujenzi wa uwanja wa michezo.

> Kenya ni nchi ya kwanza Afrika Mashariki kutumia teknolojia hii


Sagar Saghani, mwanakandarasi anayekarabati uwanja wa michezo wa Embu ambao utaandaa siku kuu ya Madaraka.

Saghani alisema kwamba uwanja huo utakuwa na uwezo wa wageni mashuhuri 1,800. Alisema ana Imani kwamba atatimiza muda ambao amepatiwa na serikali kukamilisha uwanja huo kwa wakati.

Mwanakandarasi huyo ambaye pia alipatiwa kandarasi ya kujenga uwanja wa michezo wa Kirigiti kaunti ya Kiambu, alisema atakabidhi serikali ya kitaifa nay a kaunti ya Embu uwanja huo mnamo Mei 20.

"Tekinolojia hii ni ya haraka na tutakamilisha ujenzi wa uwanja huo na kuukabidhi serikali ya kitaifa na serikali ya kaunti ya Embu kufikia Mei 20," alisema.

Alisema kwamba uwanja huo utakuwa na uwezo wa kuketi watu 8000. Aliongeza kuwa utakuwa na malango sita ya umma na moja ya watu mashuhuri.

Mwanakandarasi huyo anayemiliki kampuni ya Modern Precast K Limited aliahidi kurekebisha mfumo wa kuondoa maji katika uwanja huo ambao wakazi wa Embu wamekuwa wakilalamika.

# Waziri ahimiza nchi za Commonwealth kuondoa vikwazo vya kibiashara

NA BERNADETTE KHADULI(KNA)


Waziri wa Mashauri ya Nchi za Kigeni Dkt Alfred Mutua akihutubia mkutano wa 22 wa Mawaziri wa Mashauri ya Nchi za Kigeni wa Jumuiya ya Madola (CFAMM) katika makao makuu ya Jumuiya hiyo, Marlborough House, London.

Waziri wa Mashauri ya Kigeni na Masuala ya Wakenya wanaoishi ng'ambo Alfred Mutua anaomba vikwazo vinavyozuia usafirishaji wa bidhaa na watu miongoni mwa mataifa wanachama wa Jumuiya ya Madola viondolewe.

Dkt Mutua alisema kuondolewa kwa viza na vikwazo vingine visivyo vya kibiashara kutakuwa muhimu kusawizisha biashara katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Madola. Katika taarifa, Waziri alihakikisha kujitolea kwa Kenya kushirikiana na nchi zingine, kwa misingi ya maadili ya Jumuiya ya Madola na ushirikiano wa kirafiki wenye manufaa na ambao utalinda na kuboresha maslahi na maisha ya raia wa nchi wanachama.

" Pia ninaomba mfumo wa ufadhili wa ulimwengu ubadilishwe, kuwe na utakaorahisisha na kusimamia vyema madeni miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Madola," alisema Dkt Mutua.

Waziri alisema hayo katika mkutano wa 22 wa Mawaziri wa Mashauri ya Kigeni wa Jumuiya ya Madola (CFAMM) katika makao makuu ya Jumuiya ya Madola, Marlborough House London, ambao ulihudhuriwa na mawaziri na wawakilishi kutoka katika nchi wanachama wa Jumuiya hiyo kujadili suluhu kwa changamoto sawa zinazozikabili. Mkutano wa Mawaziri wa Mashauri ya Kigeni unafanyika kila mwaka kujadili masuala ya pamoja ya Jumuiya ya Madola.

Mkutano wa mwaka huu, ulilenga kuimarisha ustahilimivu wa nchi za Jumuiya ya Madola wakati wa mizozo na kutoa jukwaa la kila mwanachama kuelezea changamoto ambazo zinazokumba nchi zao kuhusiana na mabadiliko ya tabia nchi, janga la Covid-19, na gharama ya juu ya chakula na kawi zinazotishia kuathiri amani na uthabiti.

Katika mkutano huo, Mutua akipendekeza maeneo ambayo Mataifa wanachama yanaweza kushirikiana pamoja kama mabadiliko ya tabia nchi, uchafuzi na uharibifu wa mazingira, masuala ya amani ya kikanda na usalama na hasa kukabiliana na ugaidi, ushughulikiaji wa madeni, uchaguzi na uwiano wa kitaifa.

“ Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa”

HOMA · KIKOHOZI · KUSHINDWA KUPUMUA · MAUMIVU KOONI · KUUMWA NA KICHWA

# Kenya yashukuru Italia kwa kujenga kituo cha elimu angani

NA EMMANUEL MASHA(KNA)

Kenya imeshukuru serika ya Italia kwa kuanzisha kituo cha kimataifa cha elimu ya angani nchini.

Waziri wa Ulinzi Aden Duale alisema kwamba kituo hicho, kilicho ndani ya kituo cha angani cha San Marco Luigi Broglio Ngomeni, kaunti ya Kilifi, ni kituo muhimu kwa kutoa mafunzo kwa wahandisi wa Kenya na wengine katika ukanda huu kuhusu shughuli za ardhini na angani..

Akizungumza alipoandamana na Rais wa Italia Sergio Mattarella kuzuru kituo hicho cha angani, Duale alisema Kenya itatumia uwepo wa kituo hicho kujenga uwezo wake katika tekinolojia ili kuafikia malengo yake ya maendeleo ya uchumi jamii.

Alisema kwamba kituo hicho kina nafasi muhimu katika uhusiano wa kidiplomasia wa nchi hizi mbili, na kuunda uhusiano wenye nguvu unaounganisha pamoja nchi hizi mbili. “Tunashukuru kuanzishwa kwa kituo hiki cha kimataifa cha elimu ya angani kama kituo muhimu kwa mafunzo ya wahandisi wetu na wengine kutoka ukanda huu kuhusu shughuli za ardhini na angani,” alisema. Gavana wa Kilifi Gideon Mung’aro aliomba serikali za Italia na Kenya kuhakikisha kituo cha angani cha San Marco Luigi Broglio kinanufaisha nchi zote mbili kwa usawa na kwamba jamii ya eneo hilo haitatengwa. “Kama serikali na taasisi, tunapaswa kufanya zaidi kwa watu wa eneo hili. Kituo hiki kimekuwa hapa tangu 1967 lakini ni machache yamefanywa kunufaisha jamii,” alisema.



Rais wa Italia, Sergio Mattarella (pili kulia) alakiwa na viongozi wa Kilifi, wakiongozwa na Gavana Gideon Mung'aro katika Malindi International Airport Jumatano. Picha na Emmanuel Masha


*MWALIKO WA ZABUNI*

REPUBLIC OF KENYA

KenGen
Kenya Electricity Generating Company PLC

## MWALIKO WA ZABUNI

| NA | NAMBA YA ZABUNI | MAELEZO | UHITIMU | TAREHE YA KUFUNGA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | KGN-KIP-018-2023 | Usambazaji Vifaa vya Usalama vya Umeme kwa Vituo vya Umeme vya Kipevu | Mashirika ya Vijana | Aprili 11, 2023 saa 10:00 asubuhi |
| 2 | KGN-TURK-06-2023 | Zabuni ya Usambazaji, Usakinishaji, Jaribio, na Uagizo wa Chaja za Betri 110VDC kwa Kituo cha Umeme cha Turkwel | Mashirika ya Walemavu | Aprili 12, 2023 saa 10:00 asubuhi |
| 3 | KGN-GDD-053-2023 | Zabuni ya Ukarabati wa Mfumo wa Kupambana na Moto na Ukandamizaji wa Kiwanda cha Nguvu cha Eburru ***Kutakuwa na Ziara ya Lazima ya Eneo 28 Machi, 2023 Geothermal Plaza - Olkaria kuanzia saa 10.00 asubuhi.*** | Wanawake | Aprili 11, 2023 saa 10:00 asubuhi |
| 4 | KGN-SID-04-2023 | Zabuni ya Usambazaji, Kukusanya na Kuagiza Vifaa na Samani za Kituo cha Utafiti na Maendeleo. | Makandarasi Wananchi | Aprili 11, 2023 saa 2:00 mchana |

Makampuni yanayovutiwa yanaweza kupata taarifa zaidi kutoka kwa ofisi ya Meneja Mkuu-Mfumo wa Usambazaji, Simu: **(254) (020) 3666230**, Barua pepe: **tenders@kengen.co.ke** kwa siku za kawaida za kazi kuanzia tarehe ya tangazo.
Wazabuni ambao hawawezi kupakua hati za zabuni kutoka kwa wavuti wanaweza kuzikusanya kutoka kwa Ofisi yoyote ya Usambazaji ya KenGen baada ya malipo ya ada isiyoweza kurejeshwa ya **KShs.1, 000.00** iliyolipwa kupitia Mpesa, Namba ya Biashara **400200** na **akaunti Na. 01120069076000**, kisha utume ujumbe wa MPesa kwa wafanyakazi wa ofisi ya KenGen Finance ili kutolewa risiti rasmi.

Hati hiyo pia inaweza kutazamwa na kupakuliwa kutoka kwa tovuti **www.kengen.co.ke** na mfumo wa Ununuzi wa kielektroniki **https://eprocurement.kengen.co.ke:50001/irj/portal**

***Wazabuni wanashauriwa kurejelea tovuti na ununuzi wa kielektroniki mara kwa mara kwa maelezo yoyote ya ziada /ufafanuzi/addenda. Nakala zilizopakuliwa ni BURE.***

### KUWASILISHA ZABUNI:

1. Nyaraka za zabuni lazima ziwasilishwe mtandaoni kupitia tovuti ya KenGen E-Procurement inayopatikana kwenye tovuti ya KenGen (**www.kengen.co.ke**)

2. Wazabuni wanaopenda zabuni hii **LAZIMA** wahakikishe kuwa wamesajiliwa katika Mfumo wa Ununuzi wa Kielektroniki. Tafadhali hakikisha unazingatia yafuatayo;
   - Kwa wasambazaji wanaojisajili kwa mara ya kwanza hakikisha kisanduku tiki cha ***“Ununuzi wa Umma”*** kimetiwa alama ili maelezo ya kuingia yatumwe kwa wasambazaji mara moja.
   - Hati zote Lazima zipakiwe kwa Mfumo wa SRM kupitia **https://eprocurement.kengen.co.ke:50001/irj/portal** nayopatikana katika **www.kengen.co.ke**
   - Bei zitakazowekwa chini ya kipengee cha RFx zitakuwa sawa na bei katika ratiba ya bei.

Wazabuni wanaohitaji usaidizi wa aina yoyote kuhusu jinsi ya kutoa zabuni kupitia mfumo wanashauriwa kupakua mwongozo kutoka kwa tovuti au wanaweza kuwasiliana na **eprocurement@kengen.co.ke**

**Dhamana ya Zabuni** pale inapohitajika katika fomu na kiasi kilichobainishwa na lazima iwasilishwe katika bahasha iliyofungwa na iliyoandikwa **nambari ya zabuni na maelezo ya zabuni** kabla ya tarehe ya kufungwa kwa anwani ifuatayo:

**Meneja Mkuu- Mfumo wa Usambazaji,**
**Kampuni ya Kuzalisha Umeme Kenya PLC,**
**Oorofa ya 9, KenGen Pension Plaza II,**
**Barabara ya Kolobot, Parklands,**
**P.O. Box 47936, 00100 NAIROBI**

**Kumbuka**: Dhamana Halisi ya Zabuni inapaswa kuwekwa kwenye kisanduku cha zabuni kilicho kwenye Orofa ya Chini katika KenGen, jengo la RBS kabla ya tarehe ya mwisho ya kuwasilisha.

Zabuni zitafunguliwa **mtandaoni** mara tu baada ya muda wa kufunga mbele ya wawakilishi wa wagombeaji watkaoamua kuhudhuria katika KenGen Pension Plaza II, chumba cha ufunguzi wa Zabuni, orofa ya 6.

***N/B: KenGen inazingatia viwango vya juu vya uadilifu katika shughuli zake za biashara.***
***Ripoti tabia yoyote isiyo ya kimaadili mara moja kwa huduma iliyotolewa bila kutambulisha jina.***

**1) Piga Simu Bila Malipo: 0800722626**
**2) Faksi Bila Malipo: 00800 007788**
**3) Barua Pepe: kengen@tip-offs.com**
**4) Tovuti: www.tip-offs.com**



www.wasreb.go.ke

REPUBLIC OF KENYA

WASREB
Water Services Regulatory Board

**WATER ACT 2016 , Section 139**

## TANGAZO LA UMMA

### TAARIFA KWA UMMA KUTOA MAONI KUHUSU MAOMBI YA KAWAIDA YA USHURU KWA WATOA HUDUMA YA MAJI (WSPs) WATANO (5)

Taarifa inatolewa kwa umma kwamba:
Watoa Huduma za Maji wafuatao (WSPs), ambao wanatoa huduma za maji kwa mamlaka ya leseni iliyotolewa na Bodi ya Udhibiti wa Huduma za Maji (WASREB), wametuma maombi kwa WASREB kwa ajili ya mapitio ya mara kwa mara ya ushuru:

1. Nzoia Water Services Co. Ltd (NZOWASCO)
2. Nakuru Rural Water & Sanitation Co. Ltd (NARUWASCO)
3. Murang’a South Water & Sanitation Co. Ltd (MUSWASCO)
4. Karuri Water & Sanitation Company (KAWSCO)
5. Two Rivers Water & Sanitation Co. Ltd (TRWSC)

Zaidi ya hayo, kwamba WSPs inapendekeza mapitio ya marekebisho ya ushuru ili kuwezesha huduma za maji kufanya kazi kwa urejeshaji wa gharama kamili kwa ajili ya utoaji endelevu wa huduma za maji na kukidhi masharti muhimu kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma ambayo ni pamoja na, miongoni mwa mengine, uwekezaji mdogo.

Tafadhali kumbuka kuwa, WSP itafanya mikutano ya mseto ya mashauriano ya umma; mikutano ya ana kwa ana na mikutano ya mtandaoni kama ilivyoainishwa hapa chini

| KAUNTI | Mtoa Huduma ya Maji | Eneo | | Siku Tarehe na Wakati |
|---|---|---|---|---|
| Nakuru | Nakuru Rural Water & Sanitation Co. Ltd (NARUWASCO) | Mkutano wa Kawaida | Nakuru Rural Water & Sanitation Co. Head Quarter Office , Along Stanley Mathenge Rd, Industrial area, Nakuru Town | Jumanne, Aprili 11, 2023 10 asubuhi |
| | | Kupitia mtandao | WSP kutoa viungo | |
| Murang’a | Murang’a South Water & Sanitation Co. Ltd (MUSWASCO) | Mkutano wa Kawaida | Golden Palm Hotel, Along Kenol – Murang’a Rd | Jumatano, Aprili 12, 2023 10 asubuhi |
| | | Kupitia mtandao | WSP kutoa viungo | |
| Kiambu | Karuri Water & Sanitation Company (KAWSCO) | Mkutano wa Kawaida | St Martin De Porres Catholic Church Hall, Karuri. Banana Hill, Kiambu | Alhamisi, Aprili 13, 2023 10 asubuhi |
| | | Kupitia mtandao | WSP kutoa viungo | |
| Kaunti ya Nairobi | Two Rivers Water & Sanitation Co. Ltd (TRWSC) | Mkutano wa Kawaida | Holiday Inn Hotel, Two Rivers Mall, Limuru Rd | Ijumaa, Aprili 14, 2023 10 asubuhi |
| | | Kupitia mtandao | WSP kutoa viungo | |
| Kaunti mbili (2); Bungoma na Trans Nzoia | Nzoia Water Services Co. Ltd (NZOWASCO) | Mkutano wa Kawaida | Green Valle Hotel, Off Mumias - Bungoma Rd | Jumanne, Aprili 18, 2023 10 asubuhi |
| | | Kupitia mtandao | WSP kutoa viungo | |

Washiriki wanapaswa kuketi kabla ya saa10.00 asubuhi. Utambulisho wa kibinafsi wa washiriki utahitajika. Wananchi katika maeneo husika wanakaribishwa kutoa mawasilisho ya mdomo na maandishi na kuuliza maswali yoyote yanayoweza kuhusiana na utoaji wa huduma ya maji katika maeneo yao.

Maelezo ya mapendekezo ya marekebisho ya ushuru, uwekezaji mdogo na lengo la utendaji yanaweza kupatikana katika **www.wasreb.go.ke**.
Maoni yaliyoandikwa kuhusu ombi yatatumwa kwa barua pepe **tariffs@wasreb.go.ke** au **info@wasreb.go.ke** au tuma kwa nakala ngumu kwa:

**Afisa Mkuu Mtendaji,**
**Bodi ya Udhibiti wa Huduma za Maji,**
**Jengo la NHIF, Orofa ya 5,**
**Barabara ya Ngong,**
**P.O Box 41621 -00100, NAIROBI.**

Tarehe ya mwisho ya kupokea maoni ni siku 30 kutoka tarehe ya uchapishaji huu.

**AFISA MKUU MTENDAJI**
**BODI YA USIMAMIZI WA HUDUMA ZA MAJI**

KENYA VISION 2030

***Water Services for All***

MACHi 21, 2023

# MyGov.

NAIROBI-KENYA I TOLEO No. 36/2022-2023

A PUBLICATION OF
**Government Advertising Agency**
Telposta Towers, Kenyatta Ave/ Koinange Street
P.O Box 30025-00100,
Nairobi Kenya
Telephone: (+254) 4920000 / 1
E-Mail: info@information.go.ke

## Serikali kusambaza tani 15 za mbegu za pamba kwa wakulima Nyanza

**NA CHRIS MAHANDARA NA CATHERINE NYONGESA(KNA)**

Serikali imeanza kusambaza tani 15.8 za mbegu ya pamba aina ya BT kwa wakulima maeneo ya Nyanza na Magharibi ili kuinua uzalishaji eneo hilo.

Kupitia ushirikiano wa sekta ya kibinafsi, mpango huo wa gharama ya Sh51 milioni unalenga kuvutia wakulima zaidi huku serikali ikilenga kufufua sekta hiyo ndogo.

Katibu wa Idara ya Serikali ya Viwanda Dkt Juma Mukhwana alisema mpango huo utanufaisha wakulima katika kaunti za Kisumu, Siaya, Homa Bay, Migori, Bungoma na Busia.

Alisema kwamba, wakulima hao pia watapokea kemikali bila malipo na mafunzo kuhakikisha mumea huo unashughulikiwa vyema ili mapato mazuri yapatikane. Hii, aliongeza, inalenga kuongeza uzalishaji wa pamba nchini kutoa Mali ghafi kwa viwanda vya serikali na vya kibinafsi ambavyo vimefufuliwa.

Akizungumza katika hafla ya kuzindua zoezi hilo katika Ahero kaunti ya Kisumu. Dkt Mukhwana aliongeza kuwa serikali imefufua Rivatex na viwanda kadhaa vya pamba katika maeneo ambayo



**Katibu wa Idara ya Viwanda Dkt Dr. Juma Mukhwana (kati) na mwenzake wa Ushirika Patrick Kilemi wakabidhi wakulima mbegu za pamba za BT katika Ahero Multipurpose Hall, Kisumu. Picha na Chris Mahandara.**



**Katibu wa Idara ya Viwanda Dkt. Juma Mukwana akihutubia waandishi baada ya uzinduzi.**



**Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Agriculture and Food Authority (AFA) Beatrice Nyamwanu akihutubia waandishi habari**

mumea huo unalimwa lakini kwa sababu ya uzalishaji wa chini, vituo hivyo havifanyi kazi kulingana na uwezo wake. Ili kukidhi mahitaji, viwanda hivyo, aliongeza, vinalazimika kununua pamba nje ya nchi.

Idara ya Serikali, alisema, imeanza kufungua maeneo ya viwanda katika kaunti zote 47 ambazo pamba na nguo vitapatiwa umuhimu.

"Maeneo haya ya viwanda yatahusika na utengenezaji wa pamba na mavai kubuni ajira kwa vijana," alisema.

Katibu alihimiza vijana na wanawake kutumia juhudi za kufufua mumea huo na kujiunga na manufaa yake ya kiuchumi.

Akizungumza katika hafla hiyo, Katibu wa Idara ya Ushirika Patrick Kilemi alisema kwamba mbegu zinazosambazwa kupitia vyama vya Akiba na Mikopo (SACCO's) zitasaidia kutia nguvu mfumo wa kuongeza thamani pamba nchini. Aliongeza, hii itakuwa na manufaa makubwa katika sekta ya maziwa huku mabaki ya mbegu za pamba yakitumiwa kwa uzalishaji wa chakula cha ng'ombe wa maziwa.

"Sekta nzuri ya pamba itapunguza gharama ya lita moja ya maziwa na kutusaidia kutatua uhaba wa bidhaa hiyo nchini," alisema.

Serikali, aliongeza, imejitolea kuanzisha vyama vya ushirika vyenye nguvu, sio tu kwa sekta ndogo ya pamba lakini pia kwa sekta zingine za uchumi.Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Kilimo na Chakula (AFA) Beatrice Nyamwanu alisema juhudi mpya za kufufua sekta hiyo inanuiwa kufufua sekta hiyo kuinua uzalishaji ambao kwa sasa ni tani 3, 000.

"Tukikosa kuwa na mbegu bora, sekta itaendelea kuteseka kwa kukosa mali ghafi," akasema.

"Kufikia sasa, alisema, wakulima 20, 000 wamesajiliwa kupitia vyama vya ushirika na akaongeza kuwa


## EU yatunuku JKUAT Sh110m kutekeleza miradi wa ubunifu wa dijitali katika teknolojia saidizi

**NA RIPOTA WA MYGOV**

Chuo Kikuu cha Kilimo na Tekinolojia cha Jomo Kenyatta (JKUAT), kupitia Kituo cha Utafiti na Afya ya Uti wa Mgongo na Matibabu ya Urekebishaji, Idara ya Sayansi ya Urekebishaji, kitivo cha Sayansi ya Afya, kimepokea Sh110 milioni kutoka kwa Tume ya Ulaya.

Pesa hizo zinanuiwa kutekeleza mradi kuhusu ubunifu wa dijitali katika urekebishaji na tekinolojia ya kutoa usaidizi.

Mradi huo unaoitwa: Urekebishaji kwa Wote kupitia ubunifu wa dijitali na umilisi mpya (RADIC), unalenga kubadilisha upya elimu ya urekebishaji na mafunzo



**Dkt Wallace Karuguti, Bw. Michael Oduor (Finland), Dkt. Reuben Thuo (Msimamizi, COHES), Bw. Murtonen Kari-Pekka (Mkuu wa Global Action, Finland), Dkt. Nassib Tawa.**

kote ukanda wa Afrika Mashariki na kuhakikisha wanaohitimu wako na umilisi wa taaluma husika ya urekebishaji na tekinolojia ya usaidizi inayohitajika katika ulimwengu wa dijitali ibuka. Mradi wa RADIC uko katika kituo cha Utafiti wa Afya ya Uti wa Mgongo na Matibabu ya Urekebishaji, Idara ya Sayansi ya Urekebishaji na unaongozwa na Dkt Nassib Tawa, ambaye anahusika Kenya.

Mradi huo unafanyika kutoka 2023-2026 na unaleta pamoja vyuo vikuu vinane (JKUAT, Chuo Kikuu cha Moi , Chuo Kikuu cha JAMK (Finland), Chuo Kikuu cha Rwanda, Chuo Kikuu cha Global Health Equity (Rwanda), Kilimanjaro Christian Medical College (Tanzania), Chuo Kikuu cha Serikali cha Zanzibar na Chuo Kikuu cha Hochschule Fur Gesundheit (Ujerumani).

Mradi huo utatekelezwa chini ya mpango wa Erasmus + ndani ya kauli ya kazi ya " Kujenga Uwezo katika elimu ya juu."

Kulingana na Dkt Tawa, inakadiriwa kuwa watu 2.4 bilioni kote nchini kwa sasawanaishi na hali ambazo zimenufaika na urekebishaji.

## KWA UFUPI

### Watalii wa kigeni watarajiwa kuongezeka hadi 7 milioni

Serikali ya Kenya inapanga kuongeza idadi ya watalii wanaozuru nchini kila mwaka kuwa zaidi ya milioni saba ndani ya miaka mitano ijayo.

Katibu wa Idara ya Serikali ya Utalii Bw John Ololtua anasema kwamba Kenya ilipata Sh268 bilioni kutoka kwa watalii 1.4 milioni waliotembelea nchi mwaka wa 2022 wakiwa wameongezeka kutoka 870,000 mwaka wa 2021.

Ololtuaa anasema kwamba sekta ya utalii inachangia pakubwa Pato la Nchi (GDP), akisema ongezeko la idadi ya Watalii litaongeza mapato.

Akizungumza akiwa Kakamega katika makala ya tatu la Tamasha za Utamaduni, Utalii na Chakula Kenya, Katibu alisema sehemu ya mikakati itakuwa ni kushirikisha kaunti kutambua bidhaa za kipekee za utalii kukuza na kuzivumisha kimataifa.

"Tunataka kuwa na bidhaa tofauti. Tunataka kujua kila kaunti Kenya inaweza kutoa. Tunashirikiana na Baraza la Magavana na pia magavana ili tuweze kustawisha kilicho cha kipekee katika kila kaunti," alisema.

Katibu alitaja Mwamba Unaolia wa Kakamega, Msitu wa Kitropiki wa Kakamega, Kituo cha Kitamaduni cha Nabongo Mumia, mapigano ya fahali na ya jogoo kama baadhi ya bidhaa za kipekee ambazo serikali inalenga kustawisha.

Aliongeza kusema kwamba idara ya serikali ya Utamaduni inakusanya ufahamu wa kienyeji na desturi ili kuzilinda, kuhifadhi na kuzifanya zijulikane humu nchini na kimataifa, akitoa mfano wa Ufalme wa Nabongo Mumia na falme zingine kote nchini anazosema ni ishara za utamaduni wetu na umoja zinazoweza kuunganisha watu Ili kuchochea utalii wa humu nchini, Katibu alisema kwamba, serikali kupitia mpango wa kuanzia raia wa mapato ya chini, itaweka mikakati ya kupunguza ada.

"Pia tunalenga Wakenya wanaoishi ng'ambo, tuko na Wakenya wengi ng'ambo na tunawalenga kupitia Balozi ili tuzungumze nao kuinua sifa za Kenya," alisema..

*Na Moses Wekesa (KNA)*

### Mawaziri waidhinisha mkakati wa kukuza uchumi baharini

Mawaziri wa shughuli za Ubaharia na Shughuli za Baharini kutoka ukanda wa Afrika Mashariki na Kati wameidhinisha mkakati wa pamoja wa kushughulikia changamoto zinazokabili sekta ya ubaharia katika ukanda huo.

Katika mkutano uliofanyika Livingstone, Zambia, mawaziri kutoka Kenya, Tanzania, Uganda, Zambia na Jamhuri ya Demokrasia ya Congo waliunda mbinu ya kuwezesha ukuaji wa uchumi wa baharini katika ukanda huu.

Waliungana chini ya mwavuli wa Kamati Kati ya Serikali kuhusu Ubaharia (ISCOS).

Waziri wa Madini, Uchumi wa Baharini na Masuala ya Ubaharia wa Kenya Salim Mvurya na Katibu wa Idara ya Ubaharia Bw Shadrack Mwadime waliwakikilisha Kenya katika mkutano huo wa maafisa wakuu.

"Imebainika kuwa kukabiliana na changamoto zinazoibuka katika sekta hii kunaitaji ushirikiano wa karibu miongoni mwa wadau wa kitaifa na kikanda katika sekta ya ubaharia na shughuli za baharini," alisema katibu mkuu wa ISCOS, Daniel Kiange.

Kiange aliongeza kusema kwamba: " Hivyo basi ni muhimu kwa shirika hili kuunda jukwaa ambalo wataalamu wa kitaifa na watungaji wa sera watajadili, kupendekeza, kuoanisha misimamo, kutambua nafasi za pamoja na changamoto na kupendekeza hatua katika mazingira ya kuzitatua wakiwa na mtazamo wa kikanda katika akili zao."

Wataalamu kutoka sekta ya Ubaharia katika nchi hizo tano walifanya kikao kabla ya mkutano wa mawaziri wa ISCOS na kubuni rasimu ya mwongozo wa ustawi wa Uchumi wa Baharini katika ukanda, ambao baadaye iliwasilishwa kwa mawaziri kuidhinisha.

"Tunaamini kwamba kikao hiki cha ISCOS kabla ya mkutano wa mashauriano wa mawaziri kitakuwa jukwaa ambalo matatizo ya sekta ya ubaharia yatagunduliwa na hatua za wazi kuundwa na kushughulikiwa na watungaji wa serikali kutoa mwelekeo wa sera," alisema katibu wa Idara ya Ubaharia na Shughuli za Baharini wa Kenya Bw Shadrack Mwadime.

*Na Julius Ndegwa (PCO)*

REPUBLIC OF KENYA
GAA GOVERNMENT ADVERTISING AGENCY
KENYA YEARBOOK EDITORIAL BOARD

**DESIGN AND EDITING OF MYGOV WEEKLY BY THE KENYA YEARBOOK EDITORIAL BOARD**
NHIF Building , 4th Floor, P.O. Box 34035-00100 Email: info@kenyayearbook.go.ke
Tel: 0202715390 / 0757029456 www.kenyayearbook.co.ke